Ni asubuhi tulivu katika Mji wa Nairobi baridi ikiwa kali, umande katika majani nao ukianza kutoweka, wingu lenye rangi ya manjano kuashiria jua kuchomoza likisambaa. Paul kijana Mtanzania alikuwa ameamka kutoka usingizini akiwa amekaa kitandani huku huzuni ikiwa imemtawala, mikono ameiweka mashavuni mwake.

‘’Maisha magumu nitaishi maisha haya mpaka lini?’’, Anaongea na mwenzake ambaye aliambatana nae kuingia Nchi ya Kenya kutafuta maisha. ‘’Paul tutafanikiwa ridhiki yetu ipo’’ Anasema Philemon rafiki yake Paul huku akiinuka na kukaa kitandani.

Mahali walipokuwa wakiishi walilipia kodi kwa kila mwezi ambalo ni banda lililokuwa mtaa wa Kariobangi. ‘’Sijui leo tutafanikisha kupata vibarua?’’ Anasema Paul, akionekana kukata tamaa na maisha magumu ya Mji wa Nairobi. Philemon yeye anaweka bidii ya kusonga mbele pasipo kuogopa lolote, ‘’Mimi siwezi kurudi nyumbani, hata nikirudi bado ni hali itakuwa ile ile tu’’ Anazungumza kwa hisia kubwa huku mishipa ya uso wake ikiwa imesimama.

Philemon na Paul wote walizaliwa na kupata elimu yao katika nchi ya Tanzania. ‘’Turudi nyumbani huku wasomi ni wengi’’ Yalikuwa maneno ya Paul, ‘’usiseme hivyo tuombe Mungu tu mambo yatakuwa sawa Paul,’’ anasema Philemon huku akionyesha uso wa kumpa matumaini rafiki yake.

Wakiwa wanaongea, aliyekuwa mmiliki wa lile banda walilokuwa wakiishi Paul na rafiki yake Philemon alikuwa amekuja kudai kodi akiwa kasimama mlangoni akiongea kwa hasira na sauti kubwa, ‘’Vijana fedha yangu ya kodi’’ anazungumza huku akigonga mlango kwa kishindo. Philemon anashituka wakati Paul akionekana kupoteza matumaini mara anaposikia mwenye banda lake akiwa amekuja kuchukua kodi yake. Wakati huo walikuwa hawana fedha yoyote mifukoni mwao, nao usiku walilala na njaa kwa kuwa hawakuwa na fedha wala chakula.

Wanafungua mlango na kutoka nje wakiwa na nyuso za upole, ‘’Kama hamna fedha ondokeni’’ Anaongea kwa kukalipia na ukali bila kuwapa nafasi ya kujitetea.

‘’Jioni nitakuletea’’, Anasema Philemon akiwa amepiga magoti chini. Paul yeye alikuwa si muongeaji kama ilivyo kwa Philemon, anabaki kimya na sura ya unyonge akijutia kuishi maisha ya shida katika mji wa Nairobi.

‘’Nimewaacha, jioni msiponilipa kodi yangu nitawafukuza hamjanisaidia kujenga nyumba hii’’ Anaondoka na kuwaacha wakiwa wamesimama Philemon pamoja na Paul.

‘’Philemon wewe nenda dampo ukaokote chupa, Mimi naamkia kwenye udahili wa kuomba kazi’’, anaongea kwa unyonge Paul. Paul alikuwa ana udahili asubuhi ya saa nne siku hiyo katika shirika lisilokuwa la kiserikali la kutetea haki za watoto walemavu.

‘’Najua Paul umekata tamaa na maisha haya, tupigane bila kuchoka’’ Philemon anaingiwa na ujasiri usio na kifani akiamini atapata kazi nafasi yake ipo.

Paul ana shahada ya Sayansi na jamii na Philemon ana shahada ya masuala ya Teknolojia na Mawasiliano wote walipatia shahada zao Nchini Tanzania Chuo kikuu cha Dar es Salaam.

‘’Sikutarajia kama itakuwa hivi!’’, Anasikitika na kuinamisha kichwa chini, yalikuwa maneno ya Paul ya kila siku kutokana na matarajio makubwa aliyokuwa nayo mara baada ya kuhitimu masomo yake ya shahada ya kwanza.

‘’Kapigane nafahamu unaweza’’ anasema Philemon, akimpa moyo Paul ambaye dhamira yake ya kuishi Mji wa Nairobi inakuwa imejawa na hofu na mashaka.

‘’Sawa’’ Anajibu akiwa anaenda kuchukua maji kwenye kikombe ili kunawa uso na kuondoka. Philemon anawaza kwenda kuokota makopo ili afanikishe kupata fedha ya kulipia kodi ya banda wanaloishi.

Paul anapokuwa ametoka nje na kuanza kunawa uso anaingiwa na mawazo kuwa hakuwa na fedha ya nauli ya kumtoa pale anapoishi kwenda sehemu ambayo udahili wa kuomba kazi ulifanyikia.

****

Amani inakuwa ndogo katika Mji wa Nairobi mara baada ya Magaidi kuvamia jengo kubwa la kibiashara na kulipua mabomu na kupelekea vifo na majeruhi wengi sana katika tukio hilo.

Idara ya uhamiaji katika Mji wa Nairobi ikawa makini na wageni wote waliokuwa katika Mji huo kwa kuimarisha ulinzi kwenye mitaa mbalimbali. Mji wa Nairobi ulifurika askari wa uhamiaji kila upande kukagua vibali vya wahamiaji wote kutoka nchi tofauti tofauti. Kibali cha Philemon na Paul kuishi Nchini Kenya kiliisha muda wake wiki mbili zilizokuwa zimepita.

Paul anapokuwa akinawa uso mara anawaona askari wa idara ya uhamiaji wa Mji wa Nairobi wakiwa wamesimama, anakitupa kikombe chake chini kikiwa na maji kisha anaondoka mbio hadi ndani kwa hofu.

Philemon nae anatoka mbio anaingia ndani na kufunga mlango kwa nguvu, ‘’Kuna nini?’’ Anauliza huku akihema kwa hofu na amesimama nyuma ya mlango ili wasiweze kusukuma mlango na kuingia ndani ‘’Askari wa uhamiaji’’ anajibu Paul akiwa amekaa chini mikono ameiweka kifuani.

Askari wanafika na kuangaza macho huku na kule, wanasimama na kuzungumza ‘’Hapa nafikiri hakuna raia wageni’’. Paul na Philemon wanasikia na kupatwa na uwoga huku wakitetemeka,’’Tuondoke’’ wanaondoka huku sauti za vishindo vya viatu vyao zikiendelea kusikika.

‘’Wameondoka’’ anasema Philemon kwa sauti ya chini, ‘’Dah!, Eee Mungu wangu maisha haya mpaka lini?’’ Anazungumza huku akisimama na kujikung’uta mavumbi, ‘’Tufanye haraka tuondoke’’ Aliongea Philemon huku akichukua gunia alilokuwa akitumia kuweka makopo aliyokuwa akiokota.

Paul anavaa kwa haraka na kutoka nje mkononi akiwa ameshikilia bahasha ya kaki. Alikuwa amechomekea mithili ya mtu asiye na shida yoyote, anatembea haraka ili asije kukutana na wale askari wa uhamiaji akaingia kwenye mtafaruku mkubwa.

Punde si punde Philemon nae anatoka akiwa na sandarusi lake la kumsaidia kuweka chupa anazokuwa akiokota. Mbadala wa kazi ulishindikana anaamuwa kujitoa kuwa muokota makopo huku akipigana kupata ajira ‘’Ipo siku’’ alijisemesha akilini mwake mwenyewe.

Anaupigiza mlango kwa nguvu na kuufunga kisha anaondoka. Muonekano wa Philemon haukusadifu kama alikuwa msomi mwenye shahada.